TANGAZO LA SERIKALI NA.146 la tarehe 8/3/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1)*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KOMKONGA YA MWAKA 2024

| | |
|---|---|
| Jina | 1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo La Komkonga ya mwaka, 2024 na itaanza kutumika tarehe itakayotangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| | |
| Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355 | 2. Eneo lililoanishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji. |
| | |
| Mpango katika eneo la kwenye Jedwali | 3. Mipango ya Jumla na ya Kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. |

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| |
|---|
| Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo: |
| |
| "Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira-nukta 436086, 9375309; baada ya hapo mpaka unaendelea Magharibi kwa umbali wa kilomita 4.945 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira-nukta 431322, 9376633; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 6.831 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira-nukta 433354,9382907; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 4.794 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P4 |

*Tangazo La Serikali Na. 146 (Linaendelea)*

yenye majira-nukta 437673,9380825; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 1.353 hadi kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba P5 yenye majira-nukta 437847,9379483 hadi ulipoanzia".

Dodoma,
29 Februari, 2024

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*